

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI**



**Simu:**255-732980745

**Fax:**255-732980745

**Baruapepe:**[ded@misungwidc.go.tz](mailto:ded@misungwidc.go.tz)

**Tovuti:**[www.misungwidc.go.tz](http://www.misungwidc.go.tz)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),

Kitengo cha Teknolojia,Habari,

Mawasiliano na Uhusiano

S.L.P 20

**MISUNGWI.**

---

**TAARIFA KWA UMMA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Kiseni Mabuba anawatangazia Wananchi na Wadau wote wa Maendeleo wa Wilaya ya Misungwi kwamba **tarehe 12 Septemba, 2018** siku ya Jumatano kutakuwa na Mkutano wa Baraza la Madiwani kwa ajili ya kupitisha taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya Nne kuanzia Julai 2017 hadi Juni 2018 kwa mwaka wa Fedha wa **2017/2018**.

Hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa **Na.7 ya mwaka 1982, Kifungu cha 67,(1)** na kanuni zake kinaelekeza kuhusu Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri kuwa wazi na Wananchi wote wanaruhusiwa kufika na kushiriki kwa kusikiliza mjadala wa masuala ya Baraza la Halmashauri na shughuli za miradi iliyotekelezwa kwa kipindi hicho.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri anawataarifu kuwa Mkutano wa Baraza hilo utafanyika katika Ukumbi wa **MGS HOTEL - Misungwi kuanzia saa 3.00 asubuhi**, wananchi wote mnakaribishwa sana ili kwa pamoja tuweze kuijenga Misungwi Mpya yenye fursa nyingi za Uwekezaji wa Viwanda.

**Imetolewa na:**

Thomas Lutego

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA na Uhusiano (W)**

**Misungwi**

**6 Septemba, 2018.**